HOTUBA YA KUFUNGIA KIKAO CHA SABA CHA MKUTANO WA WADAU WA ELIMU 2024

Ndugu Mgeni Rasmi

Ndugu Katibu Mkuu,

Manaibu Katibu Mkuu,

Ndugu Wakurugenzi mbali mbali,

Ndugu viongozi wastaafu,

Ndugu maafisa wa elimu mikoa na wilaya,

Ndugu wanakamati wa skuli mbali mbali,

Ndugu  wazazi,

Ndugu walimu na wanafunzi,

Ndugu viongozi na wawakilishi wa taasisi mbali mbali za kiserikali na zisizo za kiserikali,

Ndugu waandishi wa habari,

mabibi na mabwana,

Itifaki imezingatiwa

Assalamu alaykum warahmatullaahi wabarakaatuh

Awali ya yote ninapenda kumshukuru mwenyezi Mungu kwa kutuwezesha kufika hapa siku ya leo tukiwa na uzima na afya pamoja na furaha tele. Pili napenda kutoa pongezi zangu za dhati kwa washirika wote wa mkutano huu kwa uvumilivu wenu wa hali ya juu.

Ndugu Mgeni Rasmi,

Siku tatu za mkutano huu zimekua na mafanikio na mafunzo mengi, hasa kwetu sisi asasi za kiraia. Tumefunuliwa macho na kupewa mafunzo na sehemu mpya za kufanyia kazi. Hii imeakisi kauli ya " Mcheza kwao hutunzwa" sababu sisi tunaamini Wizara ya Elimu ni nyumbani kwetu!

Nduu Mgeni Rasmi,

Tukiwa Asasi za Kiraia, tunathamini fursa hii ya kushirikishwa katika utayarishaji, uchangiaji, na utoaji wa mapendekezo katika mkutano huu. Kwa mwaka wa saba sasa, Wizara imekuwa ikitupa nafasi ya kushiriki na kutoa mchango pamoja na kupaza sauti zetu katika changamoto mbali mbali zinazoikabili sekta ya elimu. Tunashukuru sana kwa ushirikishwaji huu na tunaomba umoja huu uendelezwe kwa ajili ya maendeleo ya watoto wetu na taifa letu.

Ndugu Mgeni Rasmi,

Tunatoa pongezi zetu za dhati kwa wizara ya elimu kwa kufanyia kazi mapendekezo tuliyoyatoa mwaka jana kwenye mkutano kama huu. Miongoni mwa mapendekezo hayo ni pamoja na kuboresha miundombinu ya kujifunzia kwa watoto wetu pamoja na kueka miundombinu ya kiteknolojia na kompyuta.

Ndugu Mgeni Rasmi,

Tunapongeza maendeleo yaliyopatikana chini ya uongozi wako imara pamoja na Katibu Mkuu na Manaibu wake kwa kuja na wazo la mageuzi na kuyasimamia maendeleo hayo kwa kupitia mipango iliyopangwa imara.

Tunakiri kwamba penye mafanikio, basi pia changamoto hazikosekani. Katika siku hizi tatu, pamoja na mafanikio yaliopatikana, tumekuwa tukizungumzia changamoto mbali mbali katika sekta ya elimu; ikiwemo uhaba wa madarasa, vifaa vya kufundishia hususan katika skuli za msingi na maandalizi, upungufu wa walimu katika maeneo mbali mbali, udhaifu wa miundombinu na changamoto mbali mbali za uratibu wa elimu katika ngazi mbali mbali. Yote ambayo yanapelekea matokeo yasioridhisha katika elimu ya watoto wetu hususan katika maeneo nyeti kama kusoma, kuhesabu, kuandika pamoja na masomo ya sayansi.

Tukiwa AZAKI, kutokana na mazungumzo na mijadala tulioishuhudia katika mkutano huu, tunapendekeza yafuatayo; mambo ambayo, tunaamini yatawezesha mashirikiano makubwa zaidi kwenye sekta ya elimu na kutusaidia kuchangia vizuri kwenye mipango iliyopangwa.

1- Kusamehewa au kupunguziwa kodi kwa asasi za kiraia zinazofanya kazi za ujenzi au miradi inayohusiana na skuli, hii ni changamoto kubwa tunasaidia ujenzi na maendeleo ya elimu kiujumla, kutozwa kodi kubwa na tozo nyengine katika kufanikisha jambo ambalo lina maslahi ya jamii na Taifa kunatukatisha tamaa na kutupunguza nguvu kwenye kujitolea.
2- Kutokana na ongezeko kubwa la idadi ya skuli binafsi, Wizara ya Elimu na taasisi zake ziongeze kasi ya kuziweka karibu na kuboresha mahusiano baina ya skuli za

serekali na skuli binafsi. Hii itafanya utatuzi wa matatizo mbali mbali ya kielimu kutatuliwa kwa urahisi.

3- Sasa hivi duniani taasisi za kitaifa zinaonekana kwa umuhimu wao. Basi na hapa kwetu pia tunaomba mashirika ya kimaendeleo yaangalie uwezekano wa kufanya kazi na asasi za kiraia pia katika utekelezaji wa miradi mbali mbali ili kuongeza kasi ya maendeleo na kuepuka kurejea mipango inayofanywa kwenye sekta ya elimu. Lengo ni lile lile la kuunga mkono juhudi za Serikali!

4- Tumegundua kwamba changamoto nyingi zilizozungumziwa hapa, utatuzi wake unakuwa mgumu kutokana na kukosekana kwa takwimu sahili au zilizo kamili. Hivyo basi kwa mfumo mpya wa elimu na mtaala wetu mpya wa umahiri, tunaomba kabla ya jambo lolote kufanyiwa kazi kuwe kuna taarifa za awali na takwimu kutoka utafiti/tafiti ambazo zinaonesha ukubwa wa tatizo na jinsi gani linaweza kufanyiwa kazi ili iwe rahisi kwa asasi zetu kuyafanyia kazi kutokana na mahitaji.

5- Skuli zinazochukuliwa kama skuli za majaribia kwa mtaala mpya zipatiwe vifaa na rasilimali zinazohitajika ili tuone hasa mtaala una changamoto zipi ukiwa na ukamilifu wa vifaa, walimu na mazingira rafiki ya utekelezaji.

6- Kwa upande wa uratibu, tunapongeza maendeleo lakini tunapendekeza kuwe na mikutano ya ZESC kila baada ya miezi mitatu inayozungumzia kazi tunazofanya na mikakati ya wizara ya elimu. Hii itasaidia kuongeza kasi na wigo wa tunaowafikia na kupunguza kurejea kwa wafikiwa wa miradi. Pia kuundwe kamati ndogo ndogo zinazoshughulika na maeneo muhimu kama vile Ubora wa Elimu, Maendeleo ya Walimu, Ubunifu na Mafunzo ya Kidigitali, Mambo ya fedha na uwekezaji n.k.

7- Kuna upungufu wa tathmini za ujifunzaji wa watoto wenye mahitaji maalum, upungufu wa kupima stadi za maisha na umahiri, na upimaji wa uwezo wa walimu na uwezo wao wa kufundisha. Tunaiomba Serikali izingatie kuyapa maeneo haya nafasi ya kuyafanyia kazi.

Ndugu Mgeni Rasmi,

Napenda kupongeza na kukushukuru tena kwa uongozi wako mahiri wenye upeo na kwa msaada wako mkubwa unaotupa sisi AZAKI. Tunakupongeza kwa ubunifu wako na juhudi mbali mbali unazochukua kuleta mageuzi katika sekta ya elimu ikiwemo kuunda kikosi kazi cha mageuzi ya elimu na baadae kikosi kazi cha kuchunguza changamoto zinazokabili sekta ya skuli binafsi. Tunakuombea uendelee na ujasiri wa kutatua changamoto mbali mbali na tunakuahidi sisi, Asasi za Kiraia tutaendelea kukuunga mkono kwa hali na mali.

Ndugu Mgeni Rasmi

Tunawashukuru wote walioshiriki katika mkutano huu katika siku hizi tatu kwa mawazo na michango mizuri. Tunaamini kwamba mwaka ujao tutakuja kujadili maendeleo makubwa na yenye upana zaidi.

Kwa hayo machache na kwa wingi katika utekelezaji, naomba kuwasilisha.

Mungu ibariki Zanzibar, Mungu ibariki Tanzania na Mungu libariki zoezi hili kwa ujumla.

Asanteni kwa kunisikiliza.